SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 23 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) JANUARI 2023

WANAFUNZI 1,073,941 WACHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Kairuki.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

WALIMU TUUNGE MKONO JUHUDI ZA SERIKALI KATIKA KUTOA ELIMU BORA KWA WANAFUNZI

Siku chache zilizopita, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Kairuki alitangaza kuwa wanafunzi 1, 073, 941 waliofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2022 wakiwemo wavulana 514, 846 na wasichana 559, 095 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2023.

Kama tunavyofahamu wanafunzi wanatakiwa kuanza masomo yao tarehe 9 Januari, 2023, hivyo Waziri aliwaagiza Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha maandalizi yote ikiwemo ujenzi wa miundombinu yote kwa ajili ya kuwapokea Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza mwaka, 2023 inakamilika kabla au ifikapo tarehe 24 Desemba 2022.

Waziri Kairuki pia aliwataka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kusimamia uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya Awali na Msingi na kuhakikisha uandikishwaji huo unakamilishwa ifikapo tarehe 31 Disemba 2022.

Kutokana na mikakati hiyo, ni dhahiri kuwa Serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha kila mwanafunzi anapata haki yake ya elimu kwa wakati na bila usumbufu. Hata hivyo, kila mmoja wetu anatambua kuwa hata kama mikakati na maandalizi ya kuwapokea wanafunzi yatakuwa makubwa kiasi gani, kama mwalimu hatatekeleza wajibu wake wa kutoa huduma bora kwa wanafunzi maandalizi yote hayatakuwa na faida.

Hivyo, Serikali inawategemea walimu kufanya kazi yao kwa bidii, weledi, uzalendo na kwa kuzingatia miiko na maadili ya kazi hiyo ili lengo la kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora linafikiwa. Wito wetu ni kuwa, katika mwaka huu 2023, kila mwalimu ajitahidi kuiunga mkono Serikali kwa kutekeleza wajibu wake kikamilifu katika kumlea mtoto kiakili, kimwili na kiroho ili Taifa letu liendelee kuwa na ustawi mzuri.

Kheri ya mwaka mpya

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina Nkwama

Wajumbe
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya
Zachary A. Dida

Mhariri Mkuu
Gerard Chami

Mhariri
Adili Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

KATUNI



WANAFUNZI 1,073,941 WACHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Wanafunzi 1, 073, 941 waliofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2022 wakiwemo wavulana 514, 846 na wasichana 559, 095 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2023.

Taarifa iliyotolewa Desemba 14, 2022 na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Angellah Kairuki imesema kuwa idadi ya wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza Januari 2023 imeongezeka kwa wanafunzi 166, 139 sawa na ongezeko la asilimia 18.30 ikilinganishwa na wanafunzi 907, 802 walopata alama ya kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022.

Kati ya waliofaulu na kupangiwa kujiunga na kidato cha kwanza wamo wanafunzi wenye mahitaji maalum 2, 775 sawa na asilimia 0.26 ambao kati yao wavulana ni 1, 491 na wasichana 1, 284.

Waziri alisema kuwa Uchaguzi wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza umefanyika kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Uchaguzi wa Wanafunzi (*Students Selection-Management Information System*) ulioundwa na wataalam wa TEHAMA wa Ofisi ya Rais TAMISEMI na Baraza la Mitihani la Tanzania ambapo alisema mfumo huo umekuwa na faida mbalimbali.

"Mfumo huu umesaidia Kupunguza muda unaotumika kwenye Uchaguzi wa Wanafunzi; Kupunguza gharama zinazotumika wakati wa Zoezi la Uchaguzi na Upangaji wa Wanafunzi; na Kuongeza ufanisi na uwazi katika uchaguzi wa Wanafunzi kwa maana ya kuwa kila Mwanafunzi anapangwa kwenye Shule kulingana na Mwongozo wa Uchaguzi unavyoelekeza," alisema.

Alifafanua kuwa Uchaguzi wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka, 2023 umezingatia kigezo cha ufaulu wa mtahiniwa anayechaguliwa ambapo kila mtahiniwa aliyefanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka, 2022 na kupata jumla ya alama za ufaulu kati ya 121 hadi 300 amechaguliwa na kupangiwa Shule ya Sekondari ya Serikali.

"Shule za Sekondari za Serikali walizopangiwa wanafunzi ziko katika makundi makuu mawili: Shule za Bweni na Shule za



Wanafunzi wakifanya mtihani.

WANAFUNZI 1,073,941 WACHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

Kutwa. Kwa upande wa shule za bweni, shule hizi zimegawanywa katika makundi matatu ambayo ni Sekondari za Bweni za Wanafunzi wenye ufaulu wa Juu Zaidi (Special Schools), Shule za Sekondari za bweni - Ufundi na shule za Sekondari za Bweni Kawaida. Shule za Bweni ni za Kitaifa na hivyo, zimepangiwa kupokea Wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kwa kuzingatia mgawanyo wa nafasi uliobainishwa na vigezo vilivyowekwa ili kuimarisha Utaifa," alifafanua.

Jumla ya Shule za Sekondari 4,309 zimepangiwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, kati ya hizo Shule 38 sawa na asilimia 0.88 ni shule za bweni za kitaifa na Shule 4,271 sawa na asilimia 99.12 ni shule za kutwa.

Katika kuhakikisha wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza, Darasa la Kwanza na Elimu ya Awali wanapata haki yao ya elimu ipasavyo, Waziri Kairuki alitoa maelekezo kwa viongozi wa ngazi ya Mikoa na Halmashauri.

Kwanza, alielekeza kuwa Wanafunzi wote waliochaguliwa wanaanza masomo yao tarehe 9 Januari, 2023, hivyo aliwaagiza Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha maandalizi yote ikiwemo ujenzi wa miundombinu yote kwa ajili ya kuwapokea Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza mwaka, 2023 inakamilika kabla au ifikapo tarehe 24 Desemba 2022.

Pili, aliagiza kuwa Wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na shule za bweni waripoti shuleni ifikapo tarehe 07 Januari, 2023; na kwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na shule za kutwa waripoti shuleni ifikapo tarehe 09 Januari, 2023 huku akiwaelekeza viongozi kuhakikisha Wazazi/ Walezi na Jamii wanahimizwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya, Halmashauri na Shule ili wanafunzi wote waliochaguliwa wanaandikishwa, wanahudhuria na kubakia Shuleni hadi watakapohitimu Elimu ya Sekondari.

Tatu, aliwataka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kusimamia uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya Awali na Msingi na kuhakikisha uandikishwaji huo unakamilishwa ifikapo tarehe 31 Disemba 2022.



Wanafunzi wakifanya kazi za darasani.

Wanafunzi wakiwa katika hali ya furaha.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)
COMPLETE
INDEPENDENCE
1961
Miaka 61
Ya Uhuru
9 Disemba
Mwenyekiti, Makamishna, Menejimenti na Watumishi wote wa TSC tunawatakia kheri Watanzania wote kwenye Maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara.
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

WALIMU 8,853 WASAJILIWA NA KUPEWA BARUA ZA AJIRA

Mwenyetiki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Lazaro Komba (kulia) akiongoza Mkutano wa Tume Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022. Pembeni ya Mwenyekiti ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

Na Mwandishi wetu - Dodoma.

Katika Robo ya Kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imesajili na kutoa barua za ajira kwa walimu 8,853 ambapo katika idadi hiyo walimu 4,563 ni wa Shule za Msingi na 4,290 ni wa Shule za Sekondari.

Hayo yameelezwa katika taarifa iliyowasilishwa kwenye Mkutano wa TSC Na.2/2022/2023 uliofanyika Desemba 19 – 23, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kiwete jijini Dodoma.

Taarifa ilieleza pia kwamba Tume hiyo imefanya uchambuzi wa Tange ya walimu katika Wilaya zote Tanzania Bara ambapo uchambuzi huo umeonesha kuwa kuna jumla ya walimu 266,388 ambapo idadi hiyo inahusisha walimu 177,956 wa shule za masingi na 88,432 ni wa shule za Sekondari.

Katika kipindi chicho, Tume ilifanya mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa Kielektroniki ujulikanao kama Teachers Service Management Information System (TSCMIS) tarehe 10 -13 Oktoba, 2022 mkoani Morogoro kwa kuhusisha watumishi kutoka Mikoa ya Mwanza (14), Dar es Salaam (10), Iringa (06) na Dodoma (14). Pia, Wilaya ya Morogoro (2) na Kishapu (1).

"Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uwezo Watumishi wa Tume kuhusu namna ya kutumia Mfumo wa TSCMIS ambao utarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ikiwa ni pamoja na kushughulikia Mashauri ya Nidhamu, Rufaa, Malalamiko, Mafao ya Ajira ya Mkataba na Mirathi na Pensheni ya kabla ya tarehe 1 Julai, 2004, Usajili wa Walimu na kutunza taarifa za wageni," ilieleza sehemu ya tarifa hiyo.

Taarifa hiyo iliendelea kueleza kuwa, moja ya majukumu

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa kwenye Mkutano wa Tume Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

WALIMU 8,853 WASAJILIWA NA KUPEWA BARUA ZA AJIRA

yanayotekelezwa TSC Makao Makuu ni kuchambua rufaa za Walimu ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka za Nidhamu Wilayani pamoja na malalamiko mbalimbali ya walimu.

"Katika Robo ya Kwanza, rufaa 34 zilipokelewa na kusajiliwa na rufaa 73 zilirithiwa katika mwaka wa fedha 2021/22 hivyo kuwa na jumla ya rufaa 107. Rufaa 60 zilichambuliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya rufaa kwa ajili ya kupitiwa na kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Tume Na.1/2022/23 ili kutolewa uamuzi. Aidha, rufaa 47 zimechambuliwa na kuandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Tume Na.2/2022/23 ili kutolewa uamuzi. Pia, malalamiko 15 kuhusu masuala ya rufaa na mashauri yalipokelewa na kufanyiwa kazi," taarifa hiyo ilisema.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa, uamuzi wa rufaa 60 zilizoamuliwa katika Mkutano wa Tume a Na. 1/2022/2023 uliandaliwa na kuwasilishwa kwa warufani ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu zinazotaka Warufani kupata uamuzi wa rufaa ndani ya siku 21 tangu unapotolewa.

Pamoja na hayo, taarifa hiyo ilibainisha kuwa katika kipindi hicho Wilaya 68 ziliwezeshwa kuchunguza mashauri ya nidhamu 273 ya walimu waliofunguliwa mashauri ya nidhamu ili kubaini ukweli wa tuhuma zinazowakabili na kuziwezesha Kamati za Wilaya kutoa uamuzi stahiki.

Baadhi ya wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye Mkutano wa Tume hiyo Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022 ukiwa unaendelea.

Ofisi ya Rais
Tawala za Mikoa
na Serikali za Mitaa

Miaka 61 ya Uhuru

Maendeleo ya Elimu kuanzia Uhuru hadi 2022

- Idadi ya shule za Msingi za Serikali zimeongezeka kutoka 3,270 mwaka 1961 hadi 17,181 mwaka 2022.
- Idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi 450,626 mwaka 1961 hadi wanafunzi 10,872,508 mwaka 2022. Walimu wameongezeka kutoka 9,885 mwaka 1961 hadi 167,245 mwaka 2022
- Shule za Elimu Maalum zimeongezeka kutoka 4 za wamisionari (Tabora, Buigiri, Irente na Uhuru Mchanganyiko mwaka 1961 hadi kufikia 747 mwaka 2022.
- Aidha, kuna Elimu Jumuishi katika shule zote za msingi. Idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa Shule za Msingi imeongezeka kutoka 1,000 mwaka 1961 hadi 72,492 mwaka 2022 (Wav 41,332 Was 31,160) kwa Shule za sekondari zinazotoa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa sasa maalum ni 1 na Jumuishi 127. Idadi ya wanafunzi ni 13,142 (Wav 6,422 Was 6,720) kwa mwaka 2022;
- Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 39 mwaka 1961 hadi 4,211 mwaka 2022. Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi kutoka 11,832 mwaka 1961 hadi 2,529,699 mwaka 2022. Walimu wameongezeka kutoka 764 mwaka 1961 hadi 84,700 mwaka 2022.

Imeandalaiwa na: Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Rais - TAMISEMI

ortamisemi ofisiyaraistamisemi www.tamisemi.go.tz

UTUMISHI WA UMMA NI KUFUATA TARATIBU, SHERIA NA KANUNI ZA KAZI: SILINDE

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. David Silinde amewataka watumishi wa Ofisi ya RAIS – TAMISEMI kusimamia misingi ya Kanuni, Sheria na Taratibu za Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yao kila mmoja kwenye nafasi yake.

Mhe. Silinde ameyasema hayo Desemba 23, 2022 Dodoma wakati akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo na kuwakumbusha watumishi majukumu yao sambamba na Utunzaji wa Siri, Kumbukumbu na Nyaraka katika utumishi wa umma.

Ameeleza kuwa Serikali kwa kutambua umuhimu wa kutoa huduma bora kwa wananchi hivyo, watumishi wanapaswa kutimiza jukumu hilo kwa kufuata misingi ya kazi ikiwa ni pamoja na kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma.

"Serikali inasisitiza Sheria, Kanuni, Miongozo, Taratibu, Nidhamu, Ufanisi, Uadilifu na utendaji bora wa kazi haki ikiwa ni misingi ya utendaji bora wa kazi" amesisitiza Silinde

Pia Silinde amewataka watumishi hao kutoa huduma kwa usawa kwa wananchi tunaowahudumia ili wananchi wetu waweze kujisikia amani kuhudumiwa na Serikali yao bila kuwa na vikwazo vyovyote.

Aidha, amewakumbusha watumishi kutojihusisha na

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) Mhe. David Silinde akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa OR - TAMISEMI yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) Mhe. David Silinde (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kulia) na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa OR - TAMISEMI, Bw. Marko Masaya wakati wa kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa OR - TAMISEMI yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

UTUMISHI WA UMMA NI KUFUATA TARATIBU, SHERIA NA KANUNI ZA KAZI: SILINDE

masuala ya rushwa kwa namna yeyote ile katika kuwahudumia wananchi na kuwasihi kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi dhidi ya virusi vya UKIMWI.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimaizi wa Rasilimali Watu Bw. Marko Masaya amesema jumla ya watumishi 565 wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI wamepatiwa mafunzo hayo ambayo yamefanyika kwa muda wa siku 5 na kusema watumishi ambao hawakupata mafunzo hayo kwa sababu mbalimbali utaandaliwa utaratibu ili waweze kushiriki.

Mafunzo hayo yameendeshwa na Maofisa kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI na yalifunguliwa Desemba 19, 2022 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Angellah Kairuki.

Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya Utendaji kazi pamoja na Utunzaji wa Siri, Nyaraka na Kumbukumbu katika Utumishi wa Umma. Mafunzo hayo yalifanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) Mhe. David Silinde (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa OR - TAMISEMI, Bw. Marko Masaya (wa kwanza kushoto) wakati wa kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa OR - TAMISEMI yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
Nawatakia kheri
ya Sikukuu
ya Krismas na
Mwaka Mpya
2023
Prof. Willy Komba
Mwenyekiti Ofisi ya Rais -TSC
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa Walimu

Mwenyekiti wa Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi Mwamgeni Jongo (katikati) amsikiliza mjumbe wa kamati hiyo (hayupo pichani) kwenye Kikao cha Kamati kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya TSC, Paulina Nkwama (kulia) akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya TSC kuhusu ajira na maendeleo ya walimu katika kikao cha kamati hiyo kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022.

Kikao cha Kamati ya Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022 kikiwa kinaendelea.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

Miaka 61 ya Uhuru

Ujenzi wa Shule bora kwa ajili ya kutoa Elimu bora.

www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa kwenye kikao cha Mradi wa Boost hivi karibuni.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
Nawatakia kheri
ya Sikukuu
ya Krismas na
Mwaka Mpya
2023
Mwl. Paulina M. Nkwama, ndc
Katibu Ofisi ya Rais -TSC
Tume ya Utumishi wa Walimu

NAIBU WAZIRI MASANJA ASHAURI MFUMO WA AJIRA ZA WALIMU UBORESHWE KUKABILIANA NA UHABA WA WALIMU VIJIJINI

Na Mwandishi wetu - Mwanza

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mary Masanja (Mb) ametoa mapendekezo ya kuboreshwa kwa mfumo wa ajira za walimu wa shule za msingi na sekondari ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu katika maeneo ya vijijini.

Ameyasema hayo wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri cha Mkoa wa Mwanza kilichofanyika leo katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mwanza ambapo pamoja na mambo mengine kilijadili namna ya kukabiliana na upungufu wa walimu vijijini.

Amesema ili kuwafanya walimu kubaki katika vituo vya kazi bila kuhama , ni vyema ajira zinapotoka kipaumbele kiwe kwa wale walio tayari kufanya kazi vijijini.

Amesema uwekwe utaratibu kila anayeomba ajira ya ualimu aingie mkataba na Serikali kwamba kwa miaka kumi atakaa katika kituo cha kazi bila kuhama na kuweka bayana kuwa hii itapunguza uhaba wa walimu vijijini.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ,Mhe. Adam Malima amesema ili kuboresha elimu mashuleni ni lazima kuweka utaratibu wa kufanya kwa wazazi wanaowakingia vifua wanaume wanaowapa mimba wanafunzi.

"Ni lazima tushughulike na wazazi hawa pamoja na watu wazima wasiojiheshimu wanaowaharibu wanafunzi wakiwa masomoni" amesisitiza.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Wabunge wa Mkoa wa Mwanza, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri za Jiji la Mwanza , Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali na watoa huduma mbalimbali za kijamii.

NAIBU WAZIRI MASANJA ASHAURI MFUMO WA AJIRA ZA WALIMU UBORESHWE KUKABILIANA NA UHABA WA WALIMU VIJIJINI

tume ya utumishi wa walimu tanzania
tumeyautumishiwawalimu
secretary@tsc.go.tz
www.tsc.gotz

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akimkaribisha Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (kulia) ili afungue Mkutano wa Tume Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

Mwenyetiki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Lazaro Komba akifungua Mkutano wa Tume Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

Wajumbe na washiriki wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye Sala ya Tume hiyo kabla ya kuanza Mkutano wa Tume hiyo Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

Baadhi ya wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye Mkutano wa Tume hiyo Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

Baadhi ya viongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye Mkutano wa Tume hiyo Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

Mwenyetiki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Lazaro Komba akipitia nyaraka wakati wa Mkutano wa Tume Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akichukua dondoo wakati wa Mkutano wa Tume Na. 2/2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Desemba 19 – 23, 2022.

SAUTI YA TSC
TANGAZO 21

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

Miaka 61 ya Uhuru

Ujenzi wa Reli ya Kisasa Unaendelea

www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi Jane Mtindya akiongea kwenye Kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya Maadili na Nidhamu ya TSC, Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya TSC kwa upande wa maadili na nidhamu ya walimu katika kikao cha kamati hiyo kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022.

Kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022 kikiwa kinaendelea.

Kikao cha Kamati ya Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022 kikiwa kinaendelea.

Kikao cha Kamati ya Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022 kikiwa kinaendelea.

Kikao cha Kamati ya Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 14, 2022 kikiwa kinaendelea.

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Desemba 17, 2022 ilipata Tuzo ya Mshindi wa Nafasi ya Pili kwa Utoaji wa Habari Sahihi za Wizara na Taasisi zake katika sekta mbalimbali za utekelezwaji wa majukumu ya Serikali na Miradi mbalimbali ya Umma. Tuzo hizo zimetolewa katika Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari 2022 Jijini Dar Es Salaam lililoandaliwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Idara ya Habari - MAELEZO na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali.

KAMATI YA TEHAMA YA TSC YATAKA MFUMO WA TSCMIS UANZE KUTUMIKA

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Kamati ya TEHAMA ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeshauri kuwa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume hiyo (TSCMIS) ambao umekamilika hivi karibuni uanze kutumika ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu na wadau mbalimbali.

Kamati imeshauri hayo wakati wa kikao chake kilichofanyika katika Ofisi za Katibu wa TSC Dodoma hivi karibuni ambapo wajumbe walieleza kuwa wilaya ambazo tayari zimepatiwa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo ziwekewe miundombinu kwa haraka ili zianze kuutumia.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongoza kikao cha Kamati ya TEHAMA (wajumbe hawapo pichani) kilichofanyika Desemba 8, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za TSC Mkao Makuu Dodoma.

Katika taarifa ya kikao cha Kamati hiyo ilifafanuliwa kuwa wajumbe wa kikao hicho walieleza kuwa iwapo mfumo huo hautatumika hivi karibuni ni rahisi kwa maofisa wa TSC waliopatiwa mafunzo ya kuutumia mfumo huo kusahau namna ya kuutumia, na hivyo rasilimali zilizotumika wakati wa kutoa mafunzo hayo zitakuwa zimepotea bure.

"Mfumo huu umejengwa kwa ajili ya kurahisisha huduma kwa walimu, hivyo ni vyema uanze kutumika kwa kuwa upo tayari. Tukichelewa kuanza kuutumia wale tuliowapa mafunzo watasahau, itatulazimu tuanze tena mafunzo upya na kutumia gharama nyingine zisizokuwa za lazima," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Pamoja na mfumo huo kuwa tayari kutumika, wajumbe wa kamati hiyo walitoa mapendekezo ya kufanya maboresho kwenye vipengele kadhaa ili kuongeza ufanizi wa utendajikazi wa mfumo huo na mapendekezo yote yalipokelewa na Kitengo cha TEHAMA kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa kwaza kulia) akiongoza kikao cha Kamati ya TEHAMA kilichofanyika Desemba 8, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za TSC Mkao Makuu Dodoma.

Katika kufanikisha matumizi ya mfumo huo, ilielezwa kuwa ni lazima ofisi za TSC Wilaya ziwe na miundombinu ya Mtandao wa Intaneti ambapo Kitengo cha TEHAMA kiliagizwa kuainisha mahitaji na makadirio ya gharama ya kujenga miundombinu hiyo katika ofisi zote za wilaya.

"Ili kupata mfumo wa TSCMIS ni lazima kuwe na mtandao wa Serikali kama ilivyo kwenye mfumo wa e-office. Hivyo, ni muhimu Menejimenti ya Tume iweke kipaumbele katika kuweka miundombinu ya Mtandao wa Intaneti ili huduma hiyo iweze kupatikana," ilisema taarifa hiyo.

Hata hivyo, ilielezwa kwamba katika baadhi ya Wilaya

KAMATI YA TEHAMA YA TSC YATAKA MFUMO WA TSCMIS UANZE KUTUMIKA

ambazo zinatumia majengo ya Wakurugenzi wa Halmashauri ambapo miundombinu ya Intaneti katika majengo hayo ipo, mfumo huo uanze kutumika kwa kuwa hakuna gharama za ziada zinazohitajika kuwezesha mfumo huo kufanya kazi.

Awali, akiwasilisha taarifa ya Mwendelezo wa Ujenzi wa Mfumo wa TSCMIS, Katibu wa Kamati hiyo ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA TSC, Kainda Ndasa alieleza kuwa katika Kikao Na.2/2021/22 cha Kamati hiyo kilichofanyika mwezi Septemba, 2022, Wajumbe walipendekeza kupatiwa taarifa ya mwendelezo wa Ujenzi wa mfumo wa TSCMIS katika kikao cha mwezi Desemba 2022.

Alianza kueleza kuwa Tume iliandaa fedha kwa ajili ya mwendelezo wa ujenzi wa mfumo wa huo, kazi mbayo ilifanyika Mkoani Morogoro kwa ajili ya kukamilisha moduli tatu zilizokuwa zimesalia.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa kwaza kushoto) akiongoza kikao cha Kamati ya TEHAMA kilichofanyika Desemba 8, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za TSC Mkao Makuu Dodoma.

"Timu ilikaa Morogoro kwa wiki tatu lakini haikuweza kukamilisha ujenzi kutokana na changamoto ya watumiaji kukaa muda mrefu baada ya ujenzi wa mfumo awamu ya kwanza ambapo ilitumika muda mrefu kukumbushana yaliyofanyika awali. Mwezi Julai, 2022 hadi katikati ya mwezi Agosti, 2022 timu ilikutana tena Morogoro ili kukamilisha moduli hizo ambapo ilifanya kazi hiyo kwa muda wa wiki saba. Kwa ujumla mfumo una moduli sita ambazo zilikamilika na kutoka na toleo la kwanza la mfumo ambapo moduli zote zinaweza kutumika." Taarifa ilieleza.

Mkuu wa Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa TSC ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya TEHAMA, Kainda Ndasa (wa kwaza kushoto) akitoa ufafanuzi wa jambo kwenye kikao cha kamati hiyo kilichofanyika Desemba 8, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za TSC Mkao Makuu Dodoma.

Hatua iliyofuata ni mafunzo ambayo yalifanyika kwa watumishi katika ofisi za Wilaya kutoka Mikoa minne kutoka kwa Kanda nne ambayo ni Dodoma, Dar es Salaam, Iringa na Mwanza na Wilaya ya Morogoro na Kishapu kwa Maafisa wawili (Katibu Msaidizi na Afisa Ajira/ Maadili) ambao ndio watumiaji wa mfumo. Mafunzo yalifanyika kuanzia tarehe 10-13.10.2022 kwa muda wa siku nne.

"Ilipendekezwa kuwa baada ya mafunzo, mfumo uzinduliwe na kuanza kutumika kwa miezi mitatu hadi sita. Kuna mambo mbalimbali ambayo hayakukamilika kwa awamu ya pili ikiwa ni pamoja na kuweka mahitaji mapya kwa kadri yanavyojitokeza huku mfumo ukiendelea kutumika," ilisema tarifa hiyo.

SAUTI YA TSC
TANGAZO 26

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

Miaka 61 ya Uhuru

Amani na Umoja ni Nguzo ya Maendeleo yetu

www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

Mwenyekiti wa Fedha, Utawala, Elimu na Utafiti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi Assela Luena (kushoto) amsikiliza mjumbe wa kamati hiyo (hayupo pichani) kwenye Kikao cha Kamati kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 16, 2022. Pembeni yake ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya Fedha, Utawala, Elimu na Utafiti ya TSC, Mwl. Paulina Nkwama akipitia nyaraka kwenye kikao cha kamati hiyo kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 16, 2022.

Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala, Elimu na Utafiti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 16, 2022 kikiwa kinaendelea.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga (katikati) akitoa ufafanuzi wakati wa Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala, Elimu na Utafiti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 16, 2022 kikiwa kinaendelea.

Baadhi ya wajumbe wa Kikao cha Kamati ya Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu Dodoma Desemba 16, 2022 wakipitia nyaraka za kikao hicho.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)
TSC tunawatakia Watanzania wote
Christmas
Njema
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa walimu

WALIMU 75 WAJENGEWA UWEZO LUSHOTO

Na Mwandishi wetu – Lushoto.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lushoto imekutana na walimu 75 kutoka shule sita (6) za Msingi na moja (1) ya Sekondari kutoka Kata ya Funta Bumbuli kwa lengo la kuwajengea uwezo juu ya masuala mbalimbali ya sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu.

Mafunzo hayo yaliyofanyika Dasemba 5, 2022 yaliongozwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Lushoto, Abihudi Hemba ambapo mada mbalimbali ziliwasilishwa na kujadiliwa.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Lushoto, Abihudi Hemba akiwasilisha mada kwenye kikao kazi cha kuwajengea uwezo walimu wa shule za Msingi na Sekondari katika kata ya Funta Bumbuli. Kikao kazi hicho kilifanyixzka Desemba 5, 2022 wilayani hapo.

Baadhi ya walimu wa Kata ya Funta Bumbuli Wilaya ya Lushoto wakiwa kwenye kikaokazi kilichoongozwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lushoto. Kikao kazi hicho kilifanyika Desemba 5, 2022 wilayani Lushoto.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
Tunawatakia Watanzania wote
Christimas Njema
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa walimu

WAZIRI MKENDA ATAKA WAKUU WA SHULE KUTOJIINGIZA KWENYE UDANGANYIFU WA MITIHANI

- Watumishi wa Serikali wakemewa vikali kuacha udanyanyifu wa mitihani;
- Wadanganyifu wote kwenye mitihani kukamatwa;
- Majina ya wadanganyifu na walituhumiwa kwa kuvujisha mitihani kuwekwa hadharani pindi hukumu zikitolewa na Mahakama;

  Marufuku Watoto shuleni kulala wawili kwenye kitanda kimoja; na
- Walimu watakiwa kufuata Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amekemea vikali udanyanyifu wa mitihani unaofanywa na baadhi ya watumishi wa Serikali wasio waaminifu na kuwataka Wakuu wa Shule kutojiingiza katika udanganyifu huo.

Waziri Mkenda aliyasema hayo hivi karibuni Jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 17 wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA) ambapo alisema kwa kufanya hivyo ni kuandaa Taifa ambalo litashindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Alisema mitihani imekuwa ikienda vizuri kwenye Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), isipokuwa inapokwenda shuleni kumekuwa na watu wachache sana ambao wanajihusisha na udanganyifu wa mitihani hiyo na kwamba Serikali haitavumilia udanganyifu huo.

"Anayeleta udanganyifu kwenye mitihani tutamkamata. Walimu hakikisheni mnakataa kujiingiza katika udanganyifu huo na kuongeza makini zaidi kwenye masuala ya mitihani, kwani ndicho kipimo cha ujifunzaji na ufundishaji wetu kupima uelewa." Alisisitiza Waziri Mkenda

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda

Aliongeza kuwa;"Kwa sasa kuna kesi zinaendelea kwa wale ambao walituhumiwa kwa kuvujisha mitihani na nawaahidi pindi hukumu zao zitakopotolewa na Mahakama, tutaweka majina yao hadharani ili kila mmoja asijaribu kujihusisha na udanganyifu huo."

Akizungumzia suala la malezi shuleni, Waziri Mkenda amewataka Walimu kufuata Mwongozo wa 2020 juu ya Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu na kwamba kama kuna changamoto zibainishwe.

"Tushirikiane kufanya ulinzi wa watoto, hakikisheni shuleni hawalali watoto wawili kitanda kimoja na kama kuna changamoto ya vyoo toeni taarifa kwa Mkurugenzi kuhusu changamoto hizo, lengo ni kuhakikisha kunakuwa na mazingira salama na rafiki ya utoaji elimu na kuwalinda watoto." Alisisitiza Waziri Mkenda

Aidha, aliwataka Walimu kuangalia maudhui ya vitabu vinavyoingia shuleni ili visiharibu wanafunzi lakini pia kutumia Skauti na Viongozi wa Dini katika kuendeleza malezi mazuri ya watoto shuleni.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde, aliwataka Wakuu wa Shule kufuatilia utendaji wa Walimu shuleni ili kuondoa alama F kwenye masomo wanayofundisha.

"Naendelea kusisitiza kufuatilia utendaji wa Walimu, lakini pia wanafunzi wanapoingia shuleni tuanze na kuhakikisha wanakuwa vizuri katika lugha, wanapoielewa na kuweza kuiandika inakuwa rahisi kwao kuelewa masomo." Alisisitiza Dkt. Msonde

Kwa upande wake Rais wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA), Frank Mahenge, aliishukuru Serikali kwa namna inavyoshirikiana na Umoja huo na kuiomba pamoja na kazi nzuri wanayoifanya ya kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu nchini kujenga pia nyumba za Walimu.

HAKUNA MWANAFUNZI DAR ATAKAYESHINDWA KUANZA SHULE – RC MAKALLA

Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.

Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam, Amos Makalla, amesema hakuna mwanafunzi kuanzia Shule ya Awali, Msingi wala Sekondari Jijini Dar Es Salaam atakayeshindwa kwenda shule kwa kigezo cha uhaba wa madarasa au madawati.

Makala aliyasema hayo hivi karibuni akiwa katika hafla ya utiaji saini, ambao umehusisha Serikali kupitia Shirika la Reli (TRL) na Kampuni za ubia wa CCECC na CRCC kutoka China iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Kikwete – Ikulu jijini Dar es Salaam.

Alisema baada ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa zaidi ya Shilingi Bilioni 12.3 za ujenzi wa madarasa, hakuna mtoto ambaye kamwe hatoenda shule.

"Mheshimiwa Rais, hali ya usalama ni shwari, nashukuru kwa Shilingi Bilioni 12.3 ulizotupa za kujenga madarasa 618, nikuhakikishie hakuna mtoto ambaye hatakwenda shule ifikapo mwezi Januari, 2023," alisema Makalla.

Mkuu huyo wa Mkoa wa Dar Es Salaam alisema ili kuhakikisha dhamira njema ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inatimia, tayari ameelekeza watendaji wote kuhakikisha ajenda ya ukamilishwaji wa madarasa inapewa kipaumbele, ili kabla ya mwezi Januari, 2023 madarasa yote yawe tayari na wanafunzi wasome.

Aliongeza kuwa, kwa mujibu wa Halmashauri ya Ilala makadirio ya wanafunzi watakaoanza masomo Januari mwakani, 2023 kwa shule za Awali ni 5,700, Msingi 25,400 na Kidato cha Kwanza 30,500.

Aidha, Makalla alisema Dar Es Salaam ndio Jiji la Kibiashara, na ndio wanufaika wa kwanza wa mradi wa Reli ya Umeme ya Mwendokasi (SGR) itakayosaidia sana Taifa letu kukuza uchumi wake lakini kukuza na uchumi wa mkoa mmoja mmoja kule ambako reli hii inapita. Tunakushukuru sana Mhe. Rais kwa utekelezaji wa miradi hii muhimu.

"Hivi karibuni ulinipa fursa ya kwenda kujifunza mambo ya usafi nchini Rwanda. Wanakushukuru sana kwa kufungua biashara baina ya mataifa yetu haya." Alisema na kuongeza: "Unayoyafanya Mheshimiwa Rais yameandikwa kwenye ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, chama cha siasa kazi yake ni kushika dola, unayoyafanya unatekeleza kile kilichopo kwenye ilani." Alisema Makalla.



tume ya utumishi wa walimu tanzania
tumeyautumishiwawalimu
secretary@tsc.go.tz
www.tsc.go.tz

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa wa Dar es Salaam walioshiriki hafla ya utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa miundombinu ya reli baina ya Shirik la Reli (TRL) na Kampuni ya Ubia kutoka China (CCECC na CRCC).

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania